# Learning by Ear – Climate Change

**Episode 05**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- JOSHUA (15)
- ALEX (15)
- DAN MACUMBA – MARINE BIOLOGIST (ABOUT 40)

Scene 2:

- LORNA (16)
- ALEX (15) – via phone
- DOCTOR (40)

Scene 3:

- LORNA (16)
- CAROL (14)
- JOSHUA (15)
- ALEX (15)

**Intro:**

Karibu msikilizaji kwa makala mengine ya Noa Bongo Jenga Maisha yako tukizungumzia kuhusu mabdiliko ya hali ya hewa. Mambo sasa yameanza kupamba moto huku wakereketwa wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha Umeme wakiimarisha juhudi zao za kupambana na wapinzani wao. Joshua na Alex wanakutana na pia hofu inazuka kuhusu uhusiano uliopo baina ya magonjwa mbalimbali na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa mengi zaidi endelea kuwa nasi hadi mwisho wa makala haya ya tano.

**Scene One: Beach**

**SFX ATMO:** **BEACH, WAVES**

**1. ALEX**: Afadhali mvua sasa imepusa, angalau tunaweza kutoka kwenda kutembea!

**2. JOSHUA:** Kweli,mimi pia. Tuna bahati dhoruba haikutufikia hatimaye.

**3. ALEX:** Najua. Eeee Josh, hebu tazama yale matumbawe. Nakumbukua wakati tulipokuwa wadogo tukija kuvua samaki mahala hapa, yalikuwa yakuvutia na yenye rangi nzuri za kupendeza.

.

**4. JOSHUA:** Ni kweli kabisa. Lakini sasa yamebadilika na kuwa meupe, yanaonekana yamekufa. Tazama, yule mtu ananya nini pale? Anaonekana akikata sehemu ya matumbawe!

**5. ALEX:** Wewe, wacha, huwezo kufanya hivyo!

**SFX:** **RUNNING THROUGH THE WATER**

**6. DAN MACUMBA:** Usijali. Nakata kipande kidogo tu ili nifanye uchnguzi. Naitwa Dan Macumba. Mimi ni mtaalam wa bayolojia ya viumbe wa baharini na nafanya utafiti kuhusu matumbawe haya.

**7. ALEX:** Kweli? Nachanganyikiwa au matumbawe yalikuwa na rangi tofauti?

**8. DAN MACUMBA:** Umepata. Yanakufa na ni janga kubwa.

**9. JOSHUA:** Una maana gani kusema yanakufa?

**10. DAN MACUMBA:** Matumbawe haya tunayaita ***misitu wa mvua baharini***. Takriban robo ya viumbe wote baharini huishi na kuzaana kwenye matumbawe. Hapa ndipo unapopata aina nyingi za samaki, uduvu, kamba na kadhalika..

**11. JOSHUA:** Babangu ni mvuvi, lakini mara nyingi hawezi kwenda mbali zaidi ya matumbawe haya.

**12. DAN MACUMBA:** Hiyo ni kwa sababu anataka kuwanasa samaki wakubwa. Unajua matumbawe ni muhimu sana kwa viumbe baharini. Chukua mfano wa mji wetu. Matumbawe huwa kama kinga kutulinda kutokana na dhoruba kama ile iliyotokea sasa hivi.

**13. ALEX:** Sasa kwa nini yanakufa?

**14. DAN MACUMBA:** Matumbawe huathiriwa kirahisi sana na mabadiliko ya kiwango cha joto cha maji, uwazi na asidi baharini. Ni ishara za mapema za mabadiliko ya hali ya hewa.

**15. JOSHUA:** Kwa hivyo matumbawe yanakufa kutokana na mabadiliko hayo ya hali ya hewa?

**16. DAN MACUMBA:** Ndio. Mabadiliko hayo huongeza kiwango cha joto sehemu ya juu ya bahari. Na kadri dioksidi ya kaboni inavyoongezeka angani na kunyonywa na bahari, ndivyo kiwango cha asidi kinavyoongezeka baharini. Yote haya yamesababisha matumbawe haya kupoteza rangi yake asili kama lile pale. Matumbawe yaliyopoteza rangi huwa dhaifu na ni rahisi kuambukizwa magonjwa.

**17. ALEX:** Kwa hivyo kutokana na mabadiliko haya ya hali ya hewa na kuongezeka kwa joto duniani huenda matumbawe yote yakaangamizwa?

**18. DAN MACUMBA:** Hebu tazama kipande hiki cha tumbawe nilichokikata sasa hivi. Ni cheupe, rahisi kuvunjika na hakina uhai. Kiwango cha joto kinapoongezeka kwa nyuzi moja, matumbawe hutapoteza rangi yake. Kikipanda kwa digrii mbili au tatu matumbawe huenda yakafa.

**19. JOSHUA:** Kwa hivyo kiwango cha joto cha maji haya huenda kimepanda kwa nyuzi mbili au tatu?

**20. DAN MACUMBA:** Naweza kusema hivyo. Na kwa sababu matumbawe yanakufa, inatishia uhai wa viumbe wengine wanaoishi ndani ya matumbawe haya.

**21. JOSHUA:** Samaki wote wadogo wanategemea matumbawe hadi kuwa wakubwa hawatakuwa na pahala pa. Na nadhani wavuvi wataathiriwa pia.

**22. DAN MACUMBA:** Yote yanahusiana: Mabadiliko ya hali ya hewa, na joto kuongezeka baharini. Inasikitisha kuona matumbawe haya mazuri yakifa mbele ya macho yetu! Sawa, mimi sasa nirudi kwa mahabara yangu. Hii hapa kadi yangu. Mkitaka maelezo zaidi, msisite kunipigia simu!.

**23. JOSHUA:** Asante sana, nimefurahi kuzungumza nawe.

**25. ALEX:** Je haishangazi? Wiki mbili zilizopita nilikuwa na shaka shaka kuhusu ongezeko la ujoto duniani na mabadiliko ya hali ya hewa. Lakini sasa, kila mahali ninapokwenda, kila kitu ninachokiona, kwa namna moja au nyingine kinaathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa..

**26. JOSHUA:** Najua. Ni jambo la kutisha sana, lakini tufanye kitu cha kufurahisha. Tucheze mpira!

**SFX:** **KICKING FOOTBALL**

**27. ALEX:** Hebu, shika huo mpira!

**28. JOSHUA:** **(shouting)** Chunga kuna dau nyuma yako!

**29. ALEX:** Umechelewa! Oh mungu wangu, tazama Josh, si hili ni dau la babako? Kuna tundu kubwa katika sehemu ya ubavuni.

**30. JOSHUA:** **(running)** Nini ? Tundu? Wapi?

**31. ALEX:** Hapa. Inaonekana mtu amelitoboa kwa shoka!

**32. JOSHUA:** Siamini. **(kicking boat)** Ni hayawani gani amefanya hivi?

**33. ALEX:** Tazama. Kuna ujumbe uliokomelewa kwa msumari ubavuni. **(pulling off note and reading)**

“Rudi shuleni. Futilia mbali maandamano. Utapata hasara zaidi kuliko hii ya dau wakati mwingine”

**34. JOSHUA:** Lazima awe ni mtu anayehusiana na kiwanda cha umeme. Wamejua tunaandaa maandamano wiki ijayo kupinga mradi huu.

**35. ALEX:** Oh hapana haiwezekani! Itakuwaje kama babangu anahusika na mambo haya?

**36. JOSHUA:** Ni jambo la kuudhi sana! Nitawezaje kumtazama babangu usoni?

**Scene Two: Hospital**

**SFX:** **PHONE RINGING**

**37. LORNA:** **(in a hushed voice)** Hallo?

**38. VOICE OF ALEX:** Lorna? Ni wewe? Sikusikii vizuri?

**39. LORNA:** Hallo, Alex. Niko Hospitalini ! Ndio sababu siwezi kuongea kwa sauti!

**40. ALEX:** Oh hapana . Ok, sawa tutazungumza badaye! Tunahitaji kuwa na mkutano. Nitakuelezea baadaye.

**41. LORNA:** Ok, sawa basi tutazungumza baadaye. Kwaheri!

**SFX:** **FOOTSTEPS APPROACHING**

**42. DOCTOR:** Ehhe. Tumepata majibu ya uchunguzi wa damu ya shangazi, na … ana malaria! Tutaanza matibabu mara moja!

**43. LORNA:** Oh, Mungu wangu! Atapona? Lakini hii si kawaida bwana daktari.,yeye huishi sehemu tambarare iliyo juu. Kawaida hawaugui malaria.

**44. DOCTOR:** Usijali atapona tu. Ni bahati nzuri umemleta haraka hospitalini. Siku hizi visa vya ugonjwa wa malaria miongoni mwa watu wanaoishi uwanda wa juu vinazidi kuongezeka.

**45. LORNA:** Lakini ni kwa nini?

| | |
|---|---|
| **46. DOCTOR:** | Utafiti unaonyesha kuwa hali hii inatokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Hali ya joto inazidi kuongezeka na hivyo kusababisha kupanda kwa kiwango cha joto katika sehemu za nyanda za juu. Maradhi yanayopatikana katika sehemu za joto na wadudu wanaosambaza magonjwa hayo kama vile mbu na inzi, sasa wamesambaa. |
| **47. LORNA:** | Tulifikiri kwamba kila mara tunapokwenda kuishi na shangazi yetu hatuwezi kuambukizwa malaria au kidingapopo! |
| **48. DOCTOR:** | Sawa. Sehemu hizo hazina visa vingi kama hapa mkoani pwani. Lakini inaonekana hali inazidi kuwa mbaya, hata katika sehemu za miji iliyoko nyanda za juu, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.<br>Hata hivyo shangazi yako anaweza kuondoka hospitalini kesho endapo homa itaanza kupungua. |
| **51. LORNA:** | Asanta sana daktari. |

## Scene Three: Lorna’s House

**SFX ATMO:** **TV IN BACKGROUND**

**52. LORNA:** Ok sawa! Sasa sote tumefika. Alex nini kilichokuwa kikiendelea?

**53. ALEX:** Aaah mimi na Josh tulikuwa ufuoni tukijadiliana na mwanabayolojia wa viumbe wa baharini, kisha tukaona dau la babake Josh limeharibiwa kabisa. Kulikuwa na ujumbe huu uliotundikiwa ubavuni mwa dau. hilo. **(pulls out note from pocket)**

**54. CAROL:** Ni watu hao hao.

**55. LORNA:** Kina nani hao?

**56. CAROL:** Sikutaka kulizungumzia swala hilo. Nilidhani ingetutisha na hatimaye kuvunjilia mbali jopo letu.

**57. JOSHUA:** Kulitokea nini, Carol?

**58. CAROL:** Kibanda changu cha magazeti kilichomwa siku mbili zilizopita. Pandikizi la mtu lilinijia ghafla na kunionya nisiwaharibie maisha wakubwa na kwamba tusitatize ujenzi wa kiwanda cha umeme.

**59. JOSHUA:** Lazima iwe ni watu hao hao walioharibu dau la babangu .Nimekasirika sana!

**60. CAROL:** Tulia! Lazima tufikirie kwa busara. Kutokana na ujumbe huu na yaliyompata Carol, jamaa hawa wanataka tuachane na kampeni yetu. Wanaogopa huenda tunapiga hatua za kufaulu.

**61. ALEX:** Ni sawa kusema hivyo Lorna. Lakini je tutafanyaje endepo kitu fulani kitatokea kwa mmoja wetu au familia zetu?

**62. LORNA:** Usijali Alex, hakuna chochote kitakachotokea. babako anahusika sana katika mradi huu. Tutajuaje hutoi siri zetu kwake? Hawa watu walijuaje kuhusu maandamano ya wiki ijayo?

**63. CAROL:** Kwani ulimwambia babako, Alex?

| | |
|---|---|
| **64. ALEX:** | Bila shaka sikumwambia. Najua hamniamini, lakini mimi pia sitaki mradi huu uendelee! Siwezi kuhatarisha maisha yenu! Mnapaswa kuniamini. |
| **65. JOSHUA:** | Nakuamini Alex! Lorna, huwezi kumlaumu Alex eti kwa sababu babake anahusika na mradi huu. Sasa tuache kubishana kuhusu swala hili. |
| **66. ALEX:** | Sawa lakini naogopa. Naona bora tufutilie mbali kampeini yetu! |
| **67. JOSHUA:** | Sawa. Mimi ningependa tuendelee! |
| **68. CAROL:** | Hata mimi pia! Hizo ni kura mbili dhidi ya moja. Lorna, zamu ni yako sasa! Uamuzi wote unakutegemea wewe! |

## END OF EPISODE 5

**Outro:**

Na hadi hapo ndipo tunapokamilisha kipindi hiki cha leo. Ungana nasi wakati mwengine usikie iwapo Lorna ataamua kujiondoa kwenye jopo la wanafunzi hao au ataendelea na kampeni kupinga kiwanda hicho. Mchezo huu kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa umeandikwa na Victoria Averill, na kumbuka ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtando wetu: www.dw-world.de/lbe Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa.